



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Tuesday, 19th August, 2025

Third Assembly – Fourth Session
FOURTY SEVENTH SITTING

*[The County Assembly met at 11:20a.m at the County Assembly Buildings]
[The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir) in the Chair]*

PRAYERS

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): We can all be seated, please.

[Loud Consultations]

Order please! Let us strive to maintain order, both in the chambers and in the gallery as well. You can see we have visitors today Honourable Members! Yes, Clerk?

NOTICE OF MOTION

PRIORITIZATION, IMPLEMENTATION AND AFFIRMATIVE ACTION FOR GENDER MAINSTREAMING IN
MOMBASA COUNTY

Yes, the Notice of Motion by Honourable Milka Moraa Ngare. Please issue your notice of Motion.

Hon. Ngare: Thank you, Mr. Speaker, for this opportunity to give Notice of Motion. But before I do, I see we have guests at the gallery and I would like to take this opportunity to welcome them to this House as they have come to be with us today. *Karibuni sana*. Mr. Speaker Sir, I beg to give notice of the following Motion;

THAT AWARE THAT Article 27 of the Constitution of Kenya guarantees quality and freedom from discrimination and under Sub-Article 6 to 8 specifically mandates the state to take legislative and other measures including affirmative action programmes and policies to redress any disadvantage...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Order Members! Order!

[Hon. Ngare continued]

Hon. Ngare: *...Any disadvantage suffered by individuals or groups because of past discrimination and to ensure that not more than two-thirds of the Members of elective or appointing bodies shall be of the same gender.*

FURTHER AWARE that Article 232 of the Constitution and Section 3 of the County Government's Act, number 17 of 2012 require equitable resource allocation, inclusivity and accountability in public service delivery at both national and County levels.

COGNIZANT THAT gender mainstreaming combined with targeted affirmative action is an internationally recognized strategy endorsed by the United Nations, the African Union and the National Gender and Equality Commission known as NGECE to integrate gender perspectives in all stages of policy making, budgeting, implementation and evaluation, while ensuring historically disadvantaged groups, especially women, are proactively empowered.

DEEPLY CONCERNED that despite policy progress, Mombasa County women remain underrepresented in political leadership, have lower access to formal employment, own fewer productive assets, face barriers in accessing credit and markets and remain disproportionately vulnerable to gender-based violence and harmful socio-cultural practises.

NOTING THAT the County Government of Mombasa has direct constitutional and statutory responsibility over devolved functions including health, trade, agriculture, water, social services, early childhood education and local infrastructure which provide critical entry points for affirmative action and targeted gender programming...

[Loud consultations]

[Interruption]

Mr. Speaker, please protect me from noise coming from my right. There is too much noise coming from Honourable Members...!

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): You are protected. Honourable Members, let the Member be heard in silence.

[Hon. Ngare continued]

FURTHER NOTING that other Counties including Nakuru and Kisumu have implemented gender responsive policies that incorporate procurement quarters for women-owned enterprises, targeted women's leadership training and gender-sensitive infrastructure projects resulting in measurable and socio-economic gains;

I, pray that the ASSEMBLY RESOLVES;

- 1. THAT the County Government of Mombasa within six months develops and adopts a Mombasa County gender mainstreaming and affirmative action policy and implementation framework aligned to the constitution and the County government's Act and NGECE guidelines,*
- 2. THAT the said framework shall;*

Integrate Gender Responsive Budgeting (GRB) in all County departments and agencies ensuring not less than 30 per cent of all County procurement opportunities are reserved for women, Youth and persons with disabilities in line with the public procurement and Asset Disposal Act.

A) Establish departmental gender desks to provide technical guidance, coordinate affirmative action programmes and monitor compliance

B) Provide mandatory capacity building, gender sensitivity training and women's leadership mentorship programmes for County staff, elected leaders and community-based leaders;

3. *THAT the County Executive Committee Member responsible for the gender and social services shall table before this Assembly by 30th September of each year a Mombasa County Annual Gender and Affirmative Action status report...*

[Applause]

Detailing progress, challenges and proposed interventions; And finally,

4. *THAT the County government in collaboration with civil society organisations, women groups, youth groups, faith-based institutions and the private sector shall implement countywide public awareness and community dialogue programmes to challenge harmful gender norms, prevent gender-based violence and promote inclusivity, inclusive participation in government and development.*

Thank you, Mr. Speaker.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you, Honourable Milka Moraa for your Notice of Motion. Yes, Clerk?

STATEMENT

THE IMPLEMENTATION STATUS OF THE ARDHI FUND REGULATION AND THE PLIGHT OF THE RESIDENTS OF KISAUNI SUB-COUNTY

Yes, Honourable Allen Katana please make your request for Statement?

Hon. Katana: Thank you, Honourable Speaker, for giving me this wonderful time so that I can issue this very important statement and also above all Honourable Speaker, I want to thank the Kisauni electorates who have decided to come make a follow-up of a number of issues that are really of concern to them. Therefore, Honourable Speaker, I want to make the following statement; that the implementation status of the Ardhi Fund regulation and the plight of residents of Kisauni Sub-County.

Honourable Speaker, pursuant to the provision of Standing Order No. 40. I wish to raise a statement of topical concern regarding the implementation status of the Ardhi Fund regulation which was passed by this Honourable House and the plight of residents of Kisauni Sub-County.

Honourable Speaker, the residents of Kisauni Sub-County continue to face serious challenges arising from the problem of absentee landlords despite of the passage of the Ardhi Fund Regulation by this House. There has been no visible progress on its implementation. Residents are still being forcefully evicted, Mr. Speaker from the parcel of land they have occupied for decades, yet, no intervention has been undertaken through the Fund.

Honourable Speaker, there has been no communication whatsoever from the Governor or the Department of the Land regarding the progress of implementation of the Ardhi Fund Regulation. This lack of clarity has left residents vulnerable while the intended relief and protection remain unfulfilled.

Honourable Speaker, therefore there are a number of petitions on land matters which were formally served to the Governor, some in January, 2024, seeking intervention on the matter. However, to date Honourable Speaker, no response has been received from either the Governor's office or the Department of Land. This delay continues to frustrate residents who are in dire need of assistance.

Honourable Speaker, the plight of the residents is further compounded by the fact that while some possess mother title, they are unable to raise the requisite fees needed for the subdivision of their land. In order to acquire individual titles, this has left them in a precarious position and exposed to land injustices. Honourable Speaker, I therefore urge this Honourable House to resolve that;

I, therefore seek clarification on the following;

- 1. What is the current implementation status of the Ardhi Fund regulation and what timelines have been set for its operationalization?*
- 2. Why has there been no communication from the Governor or the Department of Land regarding the implementation of the Fund, despite this House Honourable Speaker to have passed it?*
- 3. What action has been taken in response to the petition served by the residents of Kisauni Sub-County?*
- 4. What measures will County Executive take to ensure that residents of Kisauni...*

I will repeat that Honourable Speaker... what measures will County Executive take to ensure that residents of Kisauni and Mombasa County at large, who have mother titles and allotment but lack resources for sub division, can benefit from the Ardhi Fund and secure their title deeds?

Honourable Speaker, since this is an issue that affects the Kisauni and the Mombasa County at large, I seek your indulgence, to accord Members at least an opportunity to make their contributions. I thank you, Honourable Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Katana I do hear your plea and as such allow me to also give you another opportunity to now address this matter in the Kiswahili language for the benefit of the visitors in the gallery. Please, Honourable Katana? *Nakupa ruhusa tena ya kuchangia tena Mswada huu.*

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika, nikushukuru tena kwa hekima yako; ulioonelea ni vyema taarifa hii tukaweze kuijadili kama Jumba. Mheshimiwa Spika, Jumba hili linafanya kazi nyingi sana ambayo umma mkubwa wa Mombasa kwa ujumla hawajaelewa kwamba Waheshimiwa waliowapigia kura wanafanya kazi nyingi hapa ndani na kati ya zile kazi wanazofanya hawa Waheshimiwa walio hapa walileta sheria ya kusema wale watu wetu ambao ni maskwota lazima serikali yao iwasaidie kupata hati miliki ili wasiwe maskwota katika Ardhi za baba zao...

[Applause]

Mheshimiwa Spika, la kuhuzunisha ndilo limetuma hivi leo mpaka galari yetu leo imejaa. Wale watu Mheshimiwa Spika unao waona pale wana tabia ya kulala roho juu kwa sababu hawajui dakika nyengine watalala wapi kwa sababu kuna tabia ya watu wetu kufurushwa na kama nilivyo orodhesha katika maombi haya. Mheshimiwa Spika ni kwamba Jumba hili kwa hekima za hawa Waheshimiwa wenzangu tulikipitisha kwa kauli moja ya kwamba ni lazima serikali ya watu wetu ya Kaunti ikaweze kuhakikisha kwamba watu wetu watapata hati miliki lakini kufikia hivi sasa swali ni hii hazina tulioiweka kufikia sasa imefikia wapi na kama imesaidia, imesaidia nani? Ili msaidia huyu nani lini? Kwa sababu Mheshimiwa Spika tumeng'ang'ana kama wakaazi wa Kisauni, tumetafuta hata utawala ili wakaweze kuja wasikie vilio vya wananchi hawa wa Kisauni lakini utawala wakiongozwa na Mstahiki wa Gavana, idara ya Ardhi Mheshimiwa Spika wanawatesa wakaazi wetu wa Kisauni Mheshimiwa Spika sasa ombi ni kwamba ni lini hii itakuja fanya kazi kwa sababu hii kawia kawia hata yesu alipokawia waumini wengine wamepotelewa na imani. Mimi sitaki kuongea sana Mheshimiwa Spika ili niwakaribishe Waheshimiwa ambao mwenyezi mungu amewajaalia na neema na hekma kubwa wakaweze kuchangia ili mwisho wa kwisha wakaazi si wetu tu peke yake wa Kisauni lakini wa Mombasa Kaunti nzima waweze kupata natija na kupata hati miliki zao. Kwa hayo mengi Mheshimiwa Spika nikushukuru na niseme Ahsante sana.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Niweze pia kumpatia fursa Mheshimiwa Maimuna Salim aweze kuchangia.

Hon. Maimuna Salim: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kutuwezesha kufika hadi siku ya leo hapa. Pili, ninawashukuru wakaazi wa Kisauni ambao wameweza kufika katika Bunge ambalo walitutuma sisi tuweze kuwakilisha, pia ningependa kumshukuru Mheshimiwa Katana. Mheshimiwa Spika inasikitisha na ina hofu watu wamejikuta wamezaliwa hapo, wanajua hizo Ardhi ni zao lakini inasikitisha kwamba watu wa Kisauni hawana usingizi wa kulala ki vizuri. Watu wamezeekea pale, mimi nikiwa ni mmoja wao yani ninaushuhuda wa kuzungumza ambao ni wa masikitiko. Sisi kama Wabunge tuliweza kupitisha ile sheria ya *Ardhi Fund* tukijua ya kwamba kuna sehemu ambayo mimi nikiwa ni kiongozi tulikuwa tushafika mbali sana, kwa hivyo tulikuwa tunajua ile Ardhi Fund ikipita, kuna pesa kidogo zitatoka watu angaa asilimia hata kama 25 waweze kupata hatimiliki lakini ni masikitiko kila wakienda katika hizo ofisi husika wanarejeshwa hivi wakiambiwa hivi na muda unaenda Mheshimiwa Spika. Tunajua hatimiliki ndio jambo ambalo litamfanya mwananchi aweze kutoweza kuhangaika, akitaka kujenga nyumba hana pesa ataenda kwa benki aweze kuweka hatimiliki awezekupewa uhakika na pesa aweze kujiendeleza, lakini watu wa Kisauni wamefungwa mikono Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo mimi nimesimama kusema ya kwamba hii safari tumeianza, tutasonga pamoja na munajua ya kwamba mimi

sizungumzi kimzaha mzaha kuhusu mambo ya maisha. Maisha ni yetu sote, mmoja wetu pale akidhurika hata wewe kama Mheshimiwa hauwezi kulala kwa sababu kesho kwa Mwenyezi Mungu tutakuwa masuulia. Sisi wenyewe tukiona *grader* zimeingia kwa mashamba, Mheshimiwa Spika huwa kusema ukweli kuna kitu nakikumbuka. Kuna sehemu yaitwa Kalima Upepo nafikiri wanakujua wale watu wa Shanzu; tulikuwa wagonjwa mapresha yalitushika hapo, masukari yalitushika hapo yaani maradhi yote yalitushika kwa sababu ya kuona wenzetu wakivunjiwa. Mtu ameishi pale, amezekea pale, amezaa wajukuu pale leo unaona mashini ambayo mwanaadamu umetundiza umri wako wote, umechukua loni kwa ma *bank*, umechukua mkopo kwa makampuni kuweza kujiendeleza lakini ni habari za kusikitisha watu wa Kisauni hawalali kwa amani. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, hili jambo hatutalichukulia kirahisi wala hatutalichukulia ni la mtu binafsi; sisi kama Waheshimiwa wa Bunge hili la Kaunti tushirikiane tuweze kuwa sisi ni mfano bora wa kuweza kutetea kisauni na Mombasa yote Mheshimiwa Spika. Ahsanteni sana na nawaambia kwamba Mwenyezi Mungu atuwezeshe, sisi ni wachanga; kwa hivyo tutajaribu kadri ya Mwenyezi Mungu akavyo tuwezesha ili tuhakikishe nasi katika uongozi wetu tumeweka historia ya kwamba kuna watu ambao tuliweza kuwasaidia. Ahsanteni Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Mwinyi Mtoto?

Hon. Mwinyi Mtoto: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mimi kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumpa kongole Mheshimiwa mwenzangu Mheshimiwa wa Shanzu kwa kuweza kuleta hii Taarifa ndani ya Bunge. Mimi kama mmoja wa Waheshimiwa ambaye nimechaguliwa na watu wa Mwakirunge ndani ya Kisauni Sub- County. Mheshimiwa Spika, ndani ya Mwakirunge asilimia 88 ya wakaazi wa pale wanaishi kama *squatters*; kwa hivyo hili jambo lazima tulifuatilie bega kwa bega na Waheshimiwa wenzangu wa Kisauni na Mombasa kwa jumla ili tuweze kupata mwelekeo kuona kwamba wananchi wetu wamepata mwelekeo kuona kwamba wananchi wetu wamepata hati miliki na waweze kuishi bila wasiwasi. Ahsanteni sana Mheshimiwa Spika na wananchi wa Shanzu na wa Kisauni pamoja tuko pamoja na tutaendelea kushirikiana ili tuone kwamba munaishi bila hofu. Ahsanteni sana.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Bishop Madialo?

Hon. Madialo: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Pia mimi ningependa kuchukua fursa hii kuwakaribisha wananchi wa Shanzu karibuni sana. Bwana Spika kusema kweli, hili jambo la Ardhi Fund lilitokana na Gavana mwenyewe; yeye ndio alisema kwamba angependelea kuwa na Ardhi Fund na akashiriki nasi kama Bunge na nakumbuka kwamba maana jambo hilo tulilichukulia kwa uzito na pia tukawa tunafikiria ni jambo la dharura ndiposa mukikumbuka tulitoka kwa sherehe na tukaja hapa Bunge tarehe 24 Disemba kama kesho yake ni krismasi, mimi mwenyewe nilikuwa nimeenda kuzika mjomba wangu bara na nilipata ujumbe nikiwa bara. Nilizika tarehe 23 mjomba wangu ikabidi hivyo hivyo nije kwa haraka ili tukapate kupitisha jambo hili. Hii ni kwa sababu kulingana na sisi tuliunga mkono Gavana tukisema kwamba jambo hilo ambalo unalileta ni bora na natija kwa wananchi wetu lakini kinacho shangaza ni kwamba mwaka mmoja sasa hivi unaelekea baadaye hakuna jambo lolote ambalo hii Ardhi Fund imefanya. Mara nyingi hata mimi natoka Mikindani; Mikindani ni mahali pale CBD pekee yake ndio pengine watu wako na hatimiliki lakini huko kwengine kote ni watu ambao wanaishi kwa mashamba ya ambao sijui wako wapi na watu wamezaliwa mababu, mababa,

wamama mpaka sasa hivi ni wajukuu wako hapo lakini hawana hatimiliki roho zao ziko juu juu na mara nyingi sana nimeshafanya mikutano na watu mitaani, mpaka siku hizi wanasema mikutano na Waheshimiwa kuhusu mashamba ni bure tu na hii ni kwa sababu ya hili jambo.

Mimi ningependelea kuomba hivi na ningependa kumshukuru Mheshimiwa Katana kwa kuuliza maswali haya lakini ilitupate kupeleka jambo hili mbele zaidi, ningependa tulivalie njuga isiwe tu taarifa ambapo inakuwa sote na hao wanarejesha hapana, tungependelea Bunge ienuke yote kwa pamoja, iweni kitu kama *inquiry* fulani ambapo kwa Bunge yote tunaita utawala na wananchi waje waelezee. Jambo lingine, ukiweka shilingi milioni hamsini peke yake kwa Ardhi Fund na hiyo milioni 50 pia ndio itakuwa ikate katika mambo ya *administration*, shamba ni pesa ngapi? Hata hilo shamba moja, tuanze na Mikindani, Gana Hola shamba ambalo Methodist inasema ni yao na shamba hilo peke yake ni zaidi ya pengine nusu bilioni. Sasa ukiweka shilingi milioni 50 itanunua shamba gani? Kwa hivyo tunataka kwamba tuwe jambo hili tulichukulie kwa umakini maana maisha ya wananchi kuhusu mashamba si jambo la mchezo. Naunga mkono.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Allow me to give an opportunity to the Leader of the Majority. Yes, Honourable Prischilla Mumba?

[Consultations]

Members, it was the prayer of Katana that I grant three people but from the interest that am getting from the Members, I will allow each and every one of you to contribute.

[Applause]

Leader of the Majority, please contribute to the Statement. Yes, Leader of Majority?

The Leader of Majority (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika na ahsante kwa Waheshimiwa wenza. Nafikiri mumeona kidogo kumekua na dukuduku Mheshimiwa Spika; walikuwa wanasema huyo ni boss wetu, kwa hivyo yeye angekuwa wa mwisho kuzungumza afunge mjadala, lakini kwa hekima yako ninakushukuru kuwa umeona hata nikizungumza katika hakuna shida, Waheshimiwa nataka muone kuwa sote tunastahili kwa wakati wowote, *we are level and* mimi sitaki kuonyeshwa kuwa niko bora kuliku mwengine. Mheshimiwa yeyote ni bora katika Nyumba hii na nina waheshimu nyote, ahsanteni kwa kunipa hiyo heshima. Pili, ninatoa fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa kijana Katana ambayo nita sema kwa upande mwengine huyu ni kama mume wangu maana mimi nimeolewa na Mijikenda. Kwa hivyo kwanza ninampa heshima hata kama nina kofia kubwa kumlika lakini kwa heshima nikifika nyumbani mimi ni...kwa hivyo inaeleweka. Pili, ninatoa shukrani zangu za dhati kuona watu wa Shanzu ambao wamekuja hapa leo kwa sababu ya kilio cha haki maana hichi kilio cha leo ni kilio cha haki.

Mimi kwanza ninasikitika kama kiongozi, kama mama, kwa sababu jambo la kutingisha nyuma kama ardhi, hakuna mtu ambaye ana wasiwasi kama mama sababu mama ana mzigo mkubwa, mama ana ulezi, mama ana watoto, mama ana nyumba na kisha nae baba ndie aliyekuwa *provider* mkubwa wa kujenga pale mahali, anashindwa sasa familia yangu nitaipoleka wapi? Hakika ni wakati muafaka na nina shukuru Mheshimiwa Katana tena nakushukuru kwa dhati ya nafsi yangu kutokea jana nilipoona nini kinachoendelea hiyo ndio uongozi, hukuchaguliwa ucheze na wananchi na nafsi zao, ulichaguliwa upigane na haki na uwatetee. Jumba hili hawezi kuingia yule mwananchi akakaa hicho kiti ulichokaa isipokuwa wewe peke

yake na wewe amekuweka pale kwa madhumuni ili uweze kumuwakilisha kwa wakati mwafaka na huu ndio wakati muafaka Waheshimiwa wenzangu kwa watu wa Shanzu walio mchagua Katana. Tusione ati kuwa amekiuka kitu chochote, Katana *you are on the right track...*

[Applause]

Pili, ninasikitika sana kwa neno hili Mheshimiwa Spika; ni kweli sisi tulitolewa katika likizo tukaja tukapitisha Ardhi Fund hapa, tukiwa likizo mimi nikiwa ni mkristo nasimama tarehe 24 sistahili hata kutoka kwangu lakini tulikuja kwa sababu tulikuwa kwa mapenzi yetu watu wa Mombasa waweze kusaidika na wapate hati miliki wakilipiwa ardhi zao. Nataka iingie katika historia kwa sababu kumbu kumbu ya Nyumba hii huwa inaingia kwenye historia kuwa sisi katika hili Bunge la tatu, tulipitisha Ardhi Fund katika kukomboa watu wetu katika kuwalipia mashamba kwa sababu kuna pesa itakayotoka katika mfuko wa Kaunti. Kwa masikitiko ninashangaa kuona watu wa Shanzu leo wametuvamia wakilia kilio cha haki; sasa munataka sisi kama viongozi munataka tufunge mdomo Mheshimiwa Spika, si wengi watumuelewa Mheshimiwa Katana lakini nakwambia ule ukweli, Mheshimiwa Katana sasa hivi halali, Mheshimiwa Katana pengine hata tukimpeleka Port-Reitz hichi kichwa kishalipuka kidogo kwa sababu akili yake sasa hivi haifanyi sawa. *He is not himself* Mheshimiwa Spika na sikuwa nimesema ni mwenda wazimu *he is not himself because of stress...*

[Applause]

Sio upungufu wa akili, ana akili timamu ndiposa wakamchagua wakamleta hapa lakini sasa hivi ana maradhi ya *stress* kulingana na presha ya watu wake na ikiwa mtu unaona ni utani, hebu yakukute kwako ndio utaelewa Katana anapitia nini na ni juzi tu mimi nilikuwako katika afisi ya waziri wa Ardhi tukiwa na waheshimiwa wenzangu hawa wa Likoni ambao wako hapa. Kama nitakuwa nasema uongo waninukuu na hoja ni kuwa kuna mshipi unapita wa barabara ambao itakuja ya *flyover* ya daraja ambayo itavuka ipite upande wa pili wa Likoni na shida iliyokuwa pale nataka muelewe ni kuwa, ardhi zile ziko kule ambazo tayari zimeshawekwa x zinatajikana watu waondoke kwa sababu ya mradi wa serikali kuu lakini wasilipwe, walikataa na wakaungana mkono wote watu wa Likoni wakasema haiwezekani. Hata kama mradi wa serikali unapita ni wapewe kwanza *title*, wawe *compensated* kwanza Ardhi na wawe *compensated* nyumba zao lakini leo tunakuwa sasa sisi watu wa Mombasa tunachezewa mchezo ya kuwa kukiwa kuna jambo lolote iwe ni mfano tu ifinikwe, mradi upite, iambiwe ni serikali kuu....

[Applause]

Nataka kusema kwa masikitiko makubwa hapa tena nikiwa Kiongozi wa Wengi ambaye nitaongoza vuguvugu na nitaliongoza bila uwoga kwa sababu mimi ni mkongwe ndani ya hili Jumba. Nimekuwa hapa ndani ya hili Jumba nikiwa na Mheshimiwa Maimuna na Mheshimiwa Katana hauko peke yako, tutashikana bega kwa bega tuhakikishe watu wako wamepewa heshima na hadhi inayostahili. Sisi hatuko hapa kupinga mtu yeyote na sisi hatuko hapa kupinga jambo la serikali lakini pia sisi hatuko hapa kuangalia watu wa nyanyaswe na wagandamizwe na sisi tuwe ni watu wa kusema Yes, Sir! *That is gone and forgotten!* Tuko hapa kutetea watu wetu na tuko hapa kutetea na kusimama na watu wa Kisauni na wakija ni watu wa Likoni tutasimama nao na wakija ni watu wa Mvita tutasimama nao na wakija ni watu wa Changamwe tutasimama nao.

Kwa sababu watu wa Jomvu naona Mheshimiwa Oj amenionyesha mkono pale hata mimi nina kilio tutasimama kwa sababu haja yetu ni kutaka haki isimame kwa kila mtu. Hawa watu Mheshimiwa Spika ni Wakenya na wana haki ya Ardhi yao, hawa si mamluki hawa si wakimbizi sasa ikiwa hawaliowakimbizi tunasikia mpaka vitambulisho wanazo itakuwa mkenya aliyezaliwa Kenya akose hati miliki ya Ardhi....

[Applause]

Mbona mwatushangaza *my friend* tuzungumze maneno mengine msemi tuntumwa na hatukutumwa tunazungumza maneno ya haki Mheshimiwa Spika, *it is high time* Mheshimiwa Katana ukitaka maandamano tutayafanya kama hatuskizwi, mimi najua hata kulala kwa jaa siku tano wakati jaa langu lilikuwa limekataa kuondolewa na nilipokuwa sisikizwi, nililala siku tano kwenye takataka na machokora wakinipikia mpaka jaa lilitoka, mambo mazuri hayaji rahisi Mheshimiwa Katana hivi vita umeanza na hivi vita si rahisi. Mheshimiwa Spika Mungu akitujalia nafikiri sisi tuna enda *recess* itakuwa wakati mwafaka sisi kama viongozi kuandamana na Mheshimiwa Katana na kuweza kufuatilia hili jambo bega kwa bega mpaka tujue mwisho wake na Mheshimiwa Allen Katana namshukuru Mungu sana amefungua macho ya ndani ambayo ulikua pengine yalikuwa yamefungika hayaoni. Hayo macho ya ndani yazidi kufunguka Mheshimiwa Allen Katana...

[Applause]

Kwa sababu kuna watu tukiwaambia maneno katika hili Jumba wanaona kama sisi tunacheza lakini Mheshimiwa Allen Katana nakushukuru macho ya ndani ya ki roho yamefunguka...

[Applause]

Na umeanza kufanyia watu wako kazi sasa na Mwenyezi Mungu akujaze ujasiri na uendele kufanyia watu wa Shanzu Wadi haki na sisi tutakua nyuma yako. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Members, I was restraining myself to interrupt the Leader of the Majority Party because of restriction of time please allow me to give each one of you who is going to contribute to this statement less than two minutes. I will be forced to interrupt if you exceed that time limit, so I will give, they are four ladies standing and two gentlemen because of seniority purpose allow me to give an opportunity to Honourable Mwaka Bakari. I was supposed to give it to Honourable Fatma Swaleh Mote, *Kushe* but I will give it to Honourable Mwaka Bakari.

Hon. Mwaka Bakari: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kuwa kunipa nafasi hii kwa sababu mimi pia ni mkongwe kwa umri, kwa kua Jumba hili pia mimi ni mkongwe ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuchangia taarifa hii imekuja na Mheshimiwa Allen Katana kwa sababu mambo ya Ardhi ni donda sugu, ni donda sugu tuseme kwa Mkoa wa Pwani lakini mimi niko hapa Mombasa kwa Mombasa kwa jumla. Mheshimiwa Spika, kilio hiki hakiko eneo Bunge la Kisauni peke yake kiko kila mahali sisi Mombasa hapa tuna maeneo Bunge sita, mimi nasimama hapa mvuta ngozi huvutia kwake na mimi navutia kwangu eneo Bunge la Likoni. Eneo Bunge langu la Likoni kuna shida; shida ya kwanza

Waitiki Farm ilipiganiwa na mpaka ikafikia wakati wa kwamba Mstahiki aliyekua Gavana, Ali Hassan Joho akaingilia kati wakati wa Raisi Mheshimiwa Uhuru Kenyatta kwa sababu wale wanakaa kwa Waitiki Farm ni watu walala hoi, watu wanalala hata kwa mahandaki wanaambia kwamba walipie ploti lakini kwa imani ya Mstahiki Mheshimiwa Ali Hassan Joho alijipiga kifua na akasema hawatalipa Serikali ya Kuu iweze kulipa nusu na Serikali ya Kaunti ilipe nusu yule mwananchi aweze kukaa mahali pazuri na akae mahali huru. Lakini ilifikia mahali wakaambiwa haiwekani watalipa Ksh.180,000.00 kila mtu ambapo ukiona mtu mwenye ni mlala hoi yule wa Waitiki Farm amejenga chumba kimoja, choo hapo na jiko hapo. Atapata kweli Ksh.180,000.00? Hilo haliwezekani lakini kupitia Ardhi Fund nina imani kwamba ilikua ni moja wapo ambao kwamba wanaweza kupata hio natija ya kuweza kulipia hati miliki ile ili waweze kukaa kizuri.

Namba ya pili Mheshimiwa Spika, tuko na ardhi yetu ya Maweni No.203. 203 mpaka leo ni hadithi ziko mezani; sijui ziko kabatini, sijui ziko wapi kila siku ni ahadi ahadi mpaka leo wale watu wamekaa mpaka sasa hawajapata hati miliki. Namba ya tatu, kuna ardhi ya Mwastalafu hata juzi nafikiri Mheshimiwa Pamela Ojala aliweza kuongea kitu kama hicho mpaka kufikia sasa wale watu wa Mwastalafu pia kuna bwenyewe kila leo anadai miaka nenda miaka rudi kwamba ile sehemu ni yake. Mimi mwenyewe saa hii nina miaka 62, waniona? Watu wa Shanzu Wadi, 62 yaingiana kweli hapa? Yaingiana si ndio? Niko chonjo niko na miaka 62 na nikifungua macho pale mahali Mwastalafu kulikua pako vile vile. Wakaazi mimi mwenyewe tangu nilipozaliwa pako vile na leo hii bwenyewe pia anasema ni kwake. Kupitia Ardhi Fund tulipitisha kupitia mambo kama yale na iwapo ikiwa yeye ana hati miliki ama ikiwa iwapo yeye anasema ni kwake basi apambane na Kaunti na wananchi wa Mwastalafu waweze kukaa uhuru salama mpaka dakika ya sasa hatujaweza kupata...

[Applause]

Kwa hio Mheshimiwa Spika mimi nauungana na Mheshimiwa Allen Katana hili jahazi ni jahazi ni letu sote watu wa Mombasa waweze kuungana tuweze kukomboa watu wetu wa Mombasa waweze kukaa salama salmini. Ahsante Mheshimiwa Spika, shukran Bwana Allen Katana.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Members, please be guided while you are addressing just address the Honourable Speaker and the House and not the gallery please be advised. Yes, Honourable Fatma Swaleh Mote please make your contribution to the Statement.

Hon. Fatma Swaleh: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunipa fursa hii. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na Ardhi pasi na kizuizi. Mheshimiwa Spika, kwa kusema lile la ukweli mimi nauungana na kakangu, mdogo wangu Bwana Allen Katana...

[Applause]

Kwa kuweza kuleta hoja hii ambayo ni hoja nzito na ni hoja ya kusikitisha sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, kama unavyojua ama Waheshimiwa wanavyojua sisi swala la Ardhi Fund tulilipitisha kitambo sana kama Waheshimiwa wenza wanavyolalamika kwamba walitoka katika Krisimasi tukaja katika Jumba hili tukufu tukatimiza wajibu wetu kama Waheshimiwa wa Bunge la Kaunti la Mombasa, lakini Mheshimiwa wa Mombasa inasikitisha

sana tangu tuweze kupitisha hilo swala la Ardhi Fund mpaka dakika hiii hatujaona natija yeyote Mheshimiwa Spika...

[Applause]

Mheshimiwa Spika, kila mtu anajua wakati kulipokua na vurugu hapa kwetu Kenya, Raisi wetu aliweza kukaa chini akaweza kuomba *expertise* yaani wale watu wana ufahamu wa kazi. Mheshimiwa Spika, samahani na bila samahani kwa sababu yaonekana yule ambaye ameweza kupewa hiki kiti cha Ardhi Fund yeye mwenyewe kwanza aonekana hajielewi wala hajitambui Mheshimiwa Spika...

[Applause]

Ndipo sasa unaona watu wa Mombasa mpaka sasa wanahangaika; Waswahili wanasema kwamba nyege ni kunyegezana, imani ni kutiana. Sisi tushafanya wajibu wetu waibu wetu, wajibu wao wangekua wametuonesha mfano...

[Applause]

Wa kununua hata shamba moja lakini ni jambo la kusikitisha Mheshimiwa Spika. Na jambo jingine Mheshimiwa Spika ni Mombasa nzima kwa jumla mimi naomba Mheshimiwa Gavana aweze kuchukua wajuzi kwa Mheshimiwa Waziri Ali Hassan Joho...

[Applause]

Kwa sababu mimi pia kwangu nilikua na matatizo ya shamba Kwa Bulu, Soweto na jambo lingine la kusikitisha Mheshimiwa Spika kukwambia huyu alioweza kuchaguliwa hajielewi mpaka sasa hataki kuonana na wenye mashamba...

[Applause]

Maana yake tutakuja hapa tutadanya wananchi ya kwamba mutapata mutapata hao wenye mashamba wenyewe munawakimbia. Usawa mukae na wenye mashamba mtu atoe stakabadhi zake ikiwa shamba ni lake watu wajadiliane kibe...

[Applause]

Na lazima Mheshimiwa Spika nasema ni lazima wananchi wa Mombasa ambao wanaitwa maskwota wakae kwa utulivu Mheshimiwa Spika...

[Applause]

Mheshimiwa Spika, itakua ni jambo la kusikitisha sana mimi leo naenda kuomba kura, naenda kuomba kura nani? Mtu hana hata makazi ya kukaa...

[Applause]

Mheshimiwa Spika, ukiona Waheshimiwa wanafukuzwa mashinani ni mambo kama haya, sisi tutakwenda vipi kwenda kuomba kura na sisi tukisimama kila siku twaambia watu tatizo la ardhi litakwisha, tatizo la ardhi litakwisha ni miaka mingapi tangu sisi tuchaguliwe? Dadangu hapa Mheshimiwa Kiongozi wa Wengi, amesema yeye hii ni hatamu yake ya tatu na tatizo la ardhi mpaka sasa halijaondoka Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, mimi nazungumza na uchungu kwa kusema la ukweli si jambo la kushangilia ikiwa wewe walala mahali pazuri lakini kumbuka kuna siku ya hukumu, kuna yule mtu aliweza kukuchagua wewe ambae leo hii walala katika ghorofa yako kwa makini na yule mtu aliyeweza kukuchagua analala kwa wasi wasi. Mheshimiwa Spika, kuna siku ya hukumu ambayo hio siku itakua ni nzito kwetu sisi sote maana yake uongozi ni dhamana, uongozi ni amana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika wakati nilipokua naingia ndani nilisikia ndugu zangu wakisema wakitoka hapa wanaandamana mpaka kwa Mheshimiwa Gavana. Mheshimiwa Spika, itakua vyema sisi sote ambao tulioweza kuchaguliwa hapa tuweze kua mfano bora tuweze kuandamana na wananchi watukufu walioweza...

[Applause]

Kutupatia kura Mheshimiwa Spika. Ahsante sana ndugu yangu Mheshimiwa Allen Katana na vile vile Mheshimiwa Kiongozi wa Walio Wengi, Mheshimiwa Prischillah Mumba alisema wewe ni mume wake sijui ni bwanake, bwanake ni Mumba peke yake, ahsante sana.

[Laughter]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Milka Moraa Ngare.

Hon. Ngare: Ahsante sana Bwana Spika...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Please take two minutes...

Hon. Ngare: Yes, kwa kunipatia nafasi kidogo na mimi niweze kuchangia. Nampongeza jirani yangu Mheshimiwa Allen Katana kwa kuleta hii taarifa hapa, mimi pia ni mkaazi wa eneo Bunge la Kisauni hususan pale Bombo na mimi mahali ninaishi kuna familia nyingi sana ninajua hawana hati miliki wanahangaishwa wengine hata kulikua askari walikuja kuwafurusha wengine wakafariki ambao ni maajabu, mambo ya kusikitisha sana katika eneo Bunge la Likoni ile tunaita Waitiki *solution* serikali iliingilia wakati mambo kama haya yalikua yanatendeka serikali ikanunua shamba wale ambao kua wamekaa pale kwa muda wakakatiwa mashamba yao wakaanza kujenga nyumba na wamekaa raha mustarehe. Kwa sababu gani watu wa eneo Bunge la Kisauni wanahangaishwa...

[Applause]

Ni kwa sababu gani Waziri aliopewa kazi anahangaisha watu wa eneo la Kisauni na tulipitisha Ardhi Fund hapa hapa katika hili Jumba?

[Applause]

Vile Mheshimiwa Kiongozi wa Wengi, Mama Prischillah Mumba amesema na wengine mpaka Mheshimiwa Allen Katana mwenyewe amesema tulikuja hapa wakati tumetolewa nyumbani *on an emergency basis, one year down the line* hakuna kitu chochote kimetendeka. Sisi tutafanya kazi yetu ya *oversight* kwa sababu hawa wakaazi wa eneo Bunge la Kisauni kama hawatapata hati miliki hawawezi kupata hata mikopo katika benki, hawawezi kuweza kupata

usaidizi wowote wa kifedha kutoka mahali popote. Kwa hivyo wataendelea kukaa na umasikini na hatutaki watu wetu waendeleo kukaa na umasikini...

[Applause]

Watu wetu wapate hati miliki ili waweze kuinua maisha yao. Mwisho, wakati hawa watapewa hati miliki wamiliki wapya wa Ardhi hua wanalipa rates. Hizo rates zitasaidia ushuru wetu uweze kukua...

[Applause]

Kwa hivyo mimi nauunga Mheshimiwa Allen Katana mkono na kama mkaazi ambaye anakaa eneo Bunge la Kisauni ninajua na ninaona vile kina mama wanahangaika hawana hati miliki hata wakati ninaenda kuwafanyia *empowerment* nawambia sasa mumepea hii Ks.100,000.00 nenda mukaongeze nyengine kwa benki muje mufanye biashara wananiambia mama hatuna hati miliki sasa kama hatuna hati miliki hatuna cheti chochote tutaombaje mikopo? Kwa hivyo wakaazi wa eneo Bunge la Kisauni wapewe mashamba wapate hati miliki na Bwana Allen Katana tuko na wewe, wewe si mwendawazimu umeona mbele ulikuwa msemaji wa serikali lakini ulikuwa umepotea saa hii ndio umerudi sawa. Ahsanteni sana.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Hamida Noor please contribute in less than two minutes.

Hon. Noor: Thank you, Mr. Speaker for giving me this opportunity. I want to congratulate my good friend Honourable Allen Katana for bringing this statement. Mr. Speaker, as you are aware my colleagues have said we were brought back to this House to come and pass the Ardhi Fund a year ago. It is so unfortunate, Mr. Speaker to have the second city in Kenya that we in Mombasa do not have title deeds; we are still squatters in our own lands. Mr. Speaker, this is the city where the people come to view the tourists come to look at what we have but when they come to our cities and they find out that our own people after 100 years we are still squatters in our own land. I feel today that we are so saddened...

[Applause]

In the third Assembly that we have passed this Motion and yet they have not implemented Mr. Speaker! We wonder why we are doing our oversights to come and pass Motions in this House and to come and do our oversights in this House and yet we are not giving justice to our voters in the votes. Those ones who have given us votes; Mr. Speaker, I do stand with my friend firmly for what he has done today and forever that we are going to go on and we are going to have our titles with this statement that has come into this House.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Eliud Kimari

Hon. Kimari: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nianze kuwakaribisha wakaazi wa eneo Bunge la Kisauni ambao wameweza kufika katika Bunge hili siku ya leo. Mheshimiwa Spika, tangu niingie katika hili Bunge leo nasikia nikiwa na raha kweli...

[Applause]

Mheshimiwa Spika, mimi si mtu wa kusimama kila wakati kuchangia kila hoja lakini hii leo ambalo tunalizungumzia kwa hili Bunge linahusu hawa wananchi na si wananchi wa Mombasa peke yake na hata ningependa Mheshimiwa Allen Katana kama ingewezekana hapo kitambo kidogo kungefanywa *Amendment* isome, *Implementation status of the Ardhi Fund Regulation and the plight of the residence of the Mombasa County* kwa sababu Mheshimiwa Spika hili tatizo tunalozungumzia hapa liko kila mahali. Hivi juzi kama wiki tatu ama mwezi mmoja uliopita tulikua na Mwenyekiti wa Ardhi Fund pale eneo la Frere Town Wadi na Mheshimiwa Spika matatizo ambayo yako eneo Bunge la Kisauni ndio matatizo ambayo yako eneo Bunge la Nyali na tukirudi nyuma kidogo ule wakati nilizungumzia hili swala mwaka wa 2015 Kamati ya Bunge ya mashamba ilifika eneo Bunge la Nyali na walipofika eneo Bunge la Nyali walifika kwa Bulu wakaenda Wadi ya Frere Town halafu wakaenda katika Wadi ya Mkomani.

Mheshimiwa Spika, katika zile *findings* walipata *finding* ya kwanza walipata wananchi wengi hawakua na hati miliki ile ilikuwa ya kwanza. Ya pili, kuna wale walikua na hati miliki lakini kulikua na *absentee landlord* unapata miaka 20 miaka 40 lakini *landlord* hapatikani Mheshimiwa Spika na vile vile *findings* walipata Mheshimiwa Spika kulikua na zile *lease* za mashamba ya serikali ambazo ilikua imepeanwa lakini zilikuwa zime *expire* sasa lile Bunge katika ule wakati walikuja na *recommendations* wakasema ile National Lands Commission wakati ule ilikua ichunguze ijue hawa *absentees' landlords* ni kina nani? Hawa *leases* zime *expire* ni kina nani? Mheshimiwa Spika mimi ni Mwakilishi wa Wadi wa chama cha Orange Democratic Movement, ODM na tukipanda pale juu katika ngazi ya kitaifa tuko katika hii serikali tunasema ni *broadbased Government* Mheshimiwa Spika sioni ni haja gani tutakua katika *Broadbased Government* hawa wananchi sijui watajivunia nini 2027 wakisema walikua kwa *Broadbased Government* na tatizo la Ardhi halijatatuliwa...

[Applause]

Huku Mombasa kuna zile shamba ambazo ni GL *Government lands* na katika wakaazi hapa kuna wale ambao wako katika hizo *Government lands*...

[Applause]

Ni jukumu gani limechukuliwa tujue hii *Government Land* haihitaji mambo mengi, *Government land* iko kwa serikali hawa wananchi tutajuaje watagawiwa hii shamba; huyu atapata nini, huyu atapata nini na huyu atapata nini Mheshimiwa Spika. Vile vile kuna wale *absentee landlords* na ile wakati tuliketi na Mwenyekiti wa Ardhi Fund pale Frere Town, kuna wale *absentee landlords* ambao wako willing...

[Consultations]

Hapana kuna wale *absentee landlords*, lakini kuna wale wenye wako *present* lakini wako, lakini wako willing kunegotiate na serikali ili zile shamba ziweze kupatiwa ma *squatters* wako zile sehemu ni jukumu gani wamechukua kwa sababu, kati yetu kuna wale tulipeleka majina ya wale ma *landlords* ambao wanataka kuketi na serikali, waketi waonge tujue shamba moja itanunuliwa milioni tano au kumi wapatiwe. Mheshimiwa Spika ukiangalia ile milioni hamsini imetengwa tukisema hata tunataka kutatua tatizo la hawa wananchi, tutatua tatizo la wananchi wawili ama watatu na ukiangalia Mheshimiwa Spika ule nikimnukuu yule Mwenyekiti wa Ardhi

nitaongeza tu dakika moja ambayo nimekabidhiwa na Waheshimiwa wawili hapa nitaongeza. Mheshimiwa Spika, umenipoteza kidogo...

[Laughter]

Nikinukuu yale Mwenyekiti wa Ardhi alisema, “wakiketi na wale wamiliki wa Ardhi ambao wako willing kupatiana zile sehemu za shamba, hawataangalia the status yenye iko kwa ile shamba kwa sasa watarudi nyuma”, ile shamba vile ilikuwa kabla iendelezwe kwa sababu kama ni mijengo sio hao walijenga Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo kama ni shamba kwa mfano Mheshimiwa Spika kwa saa hizi kama ni *worth about* milioni ishirini, *they can negotiate to them, two or three million atleast to settle* hata kama ni wananchi 10 ama 20 *atleast to make a step*, lakini si kukuja kila siku hakuna jambo lolote ambalo limetatuliwa Mheshimiwa Spika. Ahsante sana.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): In less than one minute now yes Honourable Hamisi Mbaya? In less than one minute.

Hon. Hamisi Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii, lakini naomba uniweke sawa kama vile ulivyowaweka sawa wale wengine kwa sababu, wenzangu umewapatia zaidi ya dakika mbili, ukiniambia mimi nitumie dakika moja, naona itakuwa hujanitendea haki. Kwa hivyo naomba uniachie hio nafasi kama nitatumia mbili ni sawa na kama nitatumia moja pia ni sawa. Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono hoja hii kwa sababu, kama walivyozungumza Waheshimiwa Wenza kuhusiana na swala la Ardhi limekuwa ni donda sugu ndani ya Mombasa Kaunti Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi nimetoka kata ndogo ambayo ni kubwa kwa idadi ya jamii na vile vile ni kubwa kwa mipaka, kata ambayo ni kata ya Timbwani. Kwa sababu nimetoka kwenye kata ile, ambayo ni kubwa kwa idadi ya jamii na vile vile ni kubwa kwa mipaka, hata wakanipatia jina la utani wakaniita Baba Mjengo. Mheshimiwa Spika, kutoka ile kata ambayo nimetoka nimechaguliwa na jamii, kuna mtaa unaitwa Mwananguvuze, nimeweza kufanya mawasiliano na wale waandishi wetu ama sijui nitawaita vipi ambao tunaita makarani, ili iweze kuletwa taarifa yangu na Mwananguvuze. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika hili ni swala ambalo ni swala sugu ambapo katika ile kata ambapo nimetoka, mimi mwenyewe niko na *Statement* ambayo iko njiani kuingia kwenye House Business, ili niweze kuja kuisoma katika Bunge hili Mheshimiwa Spika.

Kwa hivyo pia tukiwa tuko kwenye hali kama hii ya kuzungumzia swala la Ardhi, naomba ile statement yangu kupitia wale waandishi wetu ama wale makarani wetu, ile nakala yangu ya kuhusiana na statement iwe itaingia katika Nyumba hii niweze kuisoma Mheshimiwa Spika, ili ndio niweze kupata ile fursa, ambayo itaingia kwenye Kamati ya Ardhi na Mwenyekiti wa Ardhi wa Bunge hili Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika kwa sasa mimi sitaweza kutoa lawama ya aina yeyote kwa sababu, *Statement* yangu haijaingia katika Nyumba hii, kwa hivyo kama nitakuwa nitatoa lawama ya aina yoyote ama kiongozi yeyote, itakuwa mimi ni muongo Mheshimiwa Spika na Nyumba hii imesimama kwa yale yote unayozungumza ni mambo ambayo yana nakiliwa. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi ningeomba wale makarani wetu waweze kuwa na ufuatilizaji, Mwenyezi Mungu akitujalia wakati tutakuwa tumetoka kwenye mapumziko Mheshimiwa Spika, ile *Statement* yangu ya watu wangu wa Mwananguvuze, iwe itakuwa nimeipata fursa ya kusoma katika Nyumba hii Mheshimiwa Spika. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Frankline Makanga?

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika na nichukue nafasi hii pia niujiunge na Waheshimiwa Wenza kumpongeza Mheshimiwa Allen Rodgers Katana, ambaye ni mwakilishi Wadi ya Shanzu na niwapongeze Wanashanzu kwa kuchagua Kiongozi mwenye akili timamu, mwenye maono na mwenye kuelewa anachokisema. Hamkukosea hata kidogo na anastahili chochote atakacho watu wa Shanzu na Kisauni mumpatie...

[Applause]

Mheshimiwa Spika, nikiungana na Waheshimiwa wenza kwanza ni jambo la kutamausha! Na swali ambalo mimi najiuliza ni kama hakukuwa na dharura ya jambo hili la mashamba kushughulikiwa, mbona tukakatizwa likizo zetu ambazo wengine tulikuwa tumeenda na familia zetu kumpumzika, tukaregeshwa kwa Bunge hili kwa kikao maalum kupitisha hii sheria...

[Applause]

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha zaidi ni kwamba, baada ya hayo yote kufanyika na kuona kauli, Mheshimiwa Spika labda hio *Mace* iangaliwe wajua huyu...

[Consultations]

Tuko sawa ahsante! Mheshimiwa Spika cha kutamausha ni kwamba, licha ya juhudi za Mwakilishi Wadi wa Shanzu kutafuta suluhu ya maswala ya mashamba kinachonisikitisha ni kwamba Mwenyekiti wa Ardhi Fund ambaye alichaguliwa ambaye ni Askofi Kidhaka badala ya haya yanayoendelea yeye kujitokeza kuzungumza tunaona katika mitandao ya kijamii alienda kuongelea Manispaa kuenda kukagua gwaride la Manispaa hii ni ishara kwamba wale wanaoteuliwa kufanya hizi kazi *either* hawaelewi wanachofaa kufanya ama kwa kimombo mazungumzo ama maneno ya Mheshimiwa Allen Katana "*incompetence*" kwa kizungu maana anajua kizungu huyu Bwana '*incompetence*' inachukua sehemu kubwa kwa wale watu ambao wamepewa nafasi za uongozi katika serikali hii.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kwa sababu ni majukumu ya kiserekali ama ya kigatuzi, katika katiba yetu ya Kenya, 2010 *Schedule 4(2)(b)*, ambayo ni namba (8) inahusiana na maswala ya mipangilio na maendeleo ya Gatuzi na moja wapo Mheshimiwa Spika ni maswala yanayohusiana na mashamba ipo pale '*land survey and mapping*' ambalo hili ni jukumu serikali yetu inafaa kuwa imefanya. Mheshimiwa Spika, kwangu hivi majuzi na nilipoingia tulipata kuna lalama kama hizo, kwamba kuna scheme ya since 1985/1986 ambayo iliweza kufanyiwa mapping na World bank na ikawa wameshindwa kutoa *title deeds*. Mheshimiwa Spika, baada ya kuleta hoja katika Bunge hili, ndio tukapata majibu kwamba imeshughulikiwa na wanatarajia kupeana hati miliki inapofika mwezi wa tisa. Mheshimiwa Spika hiki kipindi chote ni jambo ambalo hatukuwa tunajulishwa, kwa hivyo hatuelewi jee kuna njama ya watu kujinufaisha na mashamba ya wananchi ama ni nini inaendelea?

[Applause]

Mheshimiwa Spika mimi naona mbali na kuleta hii hoja na kuwaleta hawa mama zetu na baba zetu katika Bunge hili, Mheshimiwa Spika kutoka kwa kiti chako na mimi nitakuomba kwa sababu kanuni zetu za Bunge hili zinaruhusu, aletwe waziri anayehusika na mashamba kwa hili Bunge na wananchi wakae pale juu, ili maswali tutakayouliza ayajibu hapa hapa wananchi wakiskia...

[Applause]

Mheshimiwa Spika jambo hili la mashamba lisifanyiwe siasa kwa sababu, itakuwa ni vibaya leo mzazi mwenye watoto kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu amchukue, aende aache watoto ambao hawana historia ya mahali wanaishi, lakini hapa tuna viongozi ambao ni wajibu wao wamekosa kufanya wajibu wao, kile wanataka kufanya inapofika 2027 warudi tena pale kusema, tunataka muhula mwengine ili jambo tuweze kulifanyia. Jambo hili Mheshimiwa Spika halifai kufanyiwa siasa ni watu wafanye kazi saa hii ikifika 2027 watu waamue kama, hawa viongozi tulio nao nikianzia mimi Mwakilishi Wadi ni one or two term!

[Applause]

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Makanga, I want us to stick to parliamentary language here we are not in a public baraza let us not be carried by emotions and let us be parliamentary. Thank you.

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika japo sijaona kama kuna mahali nimenukuu vibaya...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Please I have guided you, just proceed now.

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo mimi nikimalizia kwamba, mimi naungana na Waheshimiwa wenza ya kwamba ugonjwa wowote unaowasumbua wananchi wa Mombasa ni ushughulikiwe sasa na sasa kama daktari kazi imekushinda ama hujui ugonjwa huu unatibiwa vipi?! Pitisha kwa daktari mwengine afanye hio kazi, apeane matibabu ugonjwa upone. Nafikiri hio imeeleweka na kama haijaeleweka, ieleweke kwamba tuko hapa kufanya kazi; anayeshindwa na kazi basi dawa ipo na dawa atainywa na wakitapika tutadunga sindano. Ahsante Mheshimiwa Spika.

[Applause]

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Member, you have already made contribution to this, are you up on a point of Order? Please give it to him.

Hon. Hamisi Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii, nikiwa niko na akili timamu, najua ya kwamba tayari nimeshachangia na kutokana na nidhamu za

Nyumba hii, ukichangia mara moja inatosha kwamba umeshachangia Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, nimesimama kuijulisha Nyumba hii ya kwamba wakati kama nimesimama nikisongea zaidi pale kwenye ile *Mace* kwanza huwa niko na akili timamu na huwa nataka kuonyesha heshima zangu za hali ya juu zaidi kwa Nyumba hii Mheshimiwa Spika...

[Applause]

Sipendi wala sijasimama kwa kuweka hofu ya aina yoyote Mheshimiwa Spika, nataka niwe mmoja wao katika wale ambao wanaheshima zaidi ndani ya Nyumba hii kwa sababu kule mahali nilipotoka waliniona niko na heshima zaidi ndipo wakaweza kunichagua niweze kuwawakilisha. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you for informing us. Yes, Honourable Maryam Baimu.

Hon. Baimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kuniona. Kwanza nimesimama kumpongeza Mheshimiwa Allen Katana kwa hii *Statement* alioleta hapa na tukaweza kuchangia. Mimi kitu naweza kuzungumza shida ya mashamba, imekuwa ni donda sugu ama shida ya Ardhi ni donda sugu Mombasa Kaunti nzima na nikiongezea tu kidogo tu kuzungumza ni kwamba mfano, eneo Wadi yangu niliyotokea ni Freretown na kusema ule ukweli mimi nilifurahi sana wakati Jumba hili lilipopitisha hio Ardhi Fund nikiwa na matumaini ni kona sehemu nne za Ardhi pale Freretown ambazo watu wa pale wamekaa kama masqwata na katika hizo sehemu nne wale landlord wa zile sehemu, walikuja tukaa na tukakubaliana na tukaenda mpaka kwa waziri ili tuweze kutatua hio shida ya Ardhi na tukakubalini ama tulifurahi ama mimi nilifurahi wakati Gavana wetu Abdulswamad Shariff Nassir alipokwenda kule Kadongo, akaenda akasimamisha yule mama wa kwanza landlord, ambaye alikuwa amekubali kuweza kuuzia serekali ya Kaunti ile ardhi, ili wale masqwota ama watu waliojenga kwenye Ardhi yake waweze kupata hati miliki.

Mimi kama Kiongozi wa Frere nilikuwa nimefurahi sana nikijua angalau Freretown wataweza kufurahia kwamba uongozi wa mama umeweza kusaidia wakaweza kupata title deed zao lakini ni jambo la kusikitisha mwaka umepita na baado wale wananchi hawajapata hati miliki na sasa katika imani zao wanauliza je huyu mama amekuja tu kukaa bure Bunge ama huyu mama ameenda kweli kutuwakilisha? Kwa hivyo mimi nimesimama kuunga mkono hii hoja, kusema ule ukweli ni wakati kama kitu tuliahaidi wananchi wetu na kama kuna kitu kwa hili Bunge lilikuja na tukapitisha wajibu ni iko kitu kiweze kufanyika ili tuwe na ile imani ama wananchi wetu wawe na imani na sisi kwamba hatukuja kulala tumekuja Bunge kuwakilisha na kufanya kazi. Kwa hivyo nimesimama kuunga mkono taarifa hii. Ahsante Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Leila?

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika naona Mheshimiwa Spika nimesimama nikizama nikizama, lakini hata wewe mwenyewe unachea unajua ukweli umenifanyisha zoezi, nashukuru kwa hilo zoezi. Mheshimiwa Spika kwanza nachukua fursa hii kuwakaribisha ndugu

zetu kutoka Kisauni na Shanzu karibuni sana katika Bunge hili. Jambo lengine Mheshimiwa Spika mimi kwa majina ninaitwa Leila Nyache na ninawakilisha Wadi ya Kipevu kutoka Changamwe Sub-County nimesimama na miguu yangu miwili kumuunga ndugu yangu Katana mkono katika hii taarifa yake aliyoleta leo kwa kweli, ni statement ya maana sana na hii ni statement ambayo inagusa sote hapa Waheshimiwa, sote inatugusa kwa sababu hii ni ya Mombasa Kaunti nzima ni Kisauni na Shanzu lakini pia ni Mombasa Kaunti hata mimi pia inanigusa ni masikitiko makubwa sana Mheshimiwa Spika, sasa hivi ni takriban mwaka mzima tangu tupitishe hoja hii ya Ardhi Fund na haijafanyiwa kazi, kusema ukweli Mheshimiwa Spika ni haki hio kweli? Ndugu zetu wale wanateseka kufurushwa mara hivi na hakuna jambo baya mtu unalala macho wazi ama unalala na wasi wasi, hata ugonjwa wa moyo wenyewe waeza ukakushika na swala kama hili la kufurushwa masqwota huku na huku sana wanaoteseka ni kina mama na watoto na wale wazee wetu wanaumia sana kwa sababu, hawana namna yoyote. Kwa hivyo sisi kama viongozi waliotuchagua pale mashinani, tutahakikisha ya kwamba tumesimama na wao, waweze kupata haki zao na tunasema hii maswala ya squarters katika Mombasa Kaunti yetu iishe...

[Applause]

Imalizike kwa sababu, tulikuja hapa na tukapitisha hoja ya kwamba watu wetu tumalize maswala ya masquarters na yale mashamba masquarters yaweze kununuliwa, ndio watu wetu waeze kuishi kwa salamu... Kwa hivyo tunaomba hilo jambo idara husika ya Ardhi, kwanzia waziri na watu wake wote, waweze kuzingatia hili jambo la masquarters na wazingatie hii hoja tuliyopitisha hapa, sio mchezo, mnasikia Waheshimiwa? Kila mtu ameamka na hisia zake. Kwa hivyo hii ni hatari sana inaelekea, kwa hivyo sisi tunaomba tu! hawa department husika pamoja na waziri wachukulie hili jambo kwa uzito sana, na sisi hatukuja hapa kucheka ama kuuza sura, tunataka tuwajulishe wananchi wetu. Hata mimi katika Wadi yangu ya Kipevu kuna watu wangu pia hawana title deed pale, na kuna watu wangu pia ambao ni *absentee landlords* pia wako pale. Kwa hivyo mimi pia nachangia pakubwa sana watu wetu waweze kupati hati miliki na waishi kwa salama. Ahsanteni sana, ahsante Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono *Statement* hii iliyokuja na ndugu yangu Mheshimiwa Katana na ninampongeza asilimia mia fil mia na ninamwambia tuko nyuma yako. Ahsante.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, the last one. There are four Members. I will start with Honourable Nusura.

Hon. Nusura Mwinyi: Ahsante sana Mheshimiwa Spika karibuni wageni kutoka Kisauni majina yangu ni Nusura Mwinyi Kimuswa nawakilisha Wadi ya Mtongwe na mimi nimesimama pia kupongeza kwa sababu hili ni swala nyeti katika Mombasa yetu kwa jumla si Kisauni peke yake wala Nyali wala Likoni peke yake ni Mombasa Kaunti yote. Mimi nataka niseme kule kwangu kulitokea shida kama hii kuna mtaa unaitwa Vitsangalaweni ni kijiji cha kutosha hivi ambacho kuna wenyeji walikua wameishi pale miaka mingi labda zaidi ya miaka mia mbili kwa sababu wenyeji wako pale, makaburi wako pale lakini kulitokea bwenyenye mmoja akaja kudai kwamba ile Ardhi ni yake na tulilingilia swala hili na nafikiri lilifika kwa wahusika wakuu. Tukaja tukaambiwa tutulie swala hili litashughulikiwa na mimi nataka niseme kwamba tuko na viongozi, tuko na waziri, tuko na Gavana wetu, tuko na waziri wetu pia Hassan Ali Joho ambaye pia alikuwa ameliingilia swala hili lakini mimi nataka niseme hili swala linatumiza wengi, kwanza nikiangalia wale watu wa pale kwangu hawana title na walikuwa wanategemea labda

wanaishi pale ili waje wapate hati miliki zao lakini kulitokea huyo bwenyenye bado kuna utata mwingi na tumesimama kidete kwa sababu tumechaguliwa na wananchi wakituleta hapa kuja kuangalia maswala yao haswa yale maswala ambayo yana waumiza wao binafsi. Kwa hivyo mimi nimesima kuunga mkono Mheshimiwa Spika. Ahsante.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Yes, Honourable Florence.

Hon. Mkanjala: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa hii nafasi. Ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa mwenzangu Honourable Katana kwa kuleta taarifa hii na naungana naunga mkono naungana mtanisameheha kidogo kiswahili yangu acha niongee kizungu kama mtaniruhusu. *I agree with the statement that he has brought that this issue of land is a really vital problem that has been an issue going on not only for Kisauni and Shanzu it is a problem that is going on around Mombasa and it is high time that the Governor or waziri in fact waziri needs to be called, he needs to account for why the Ardhi Fund has not been implemented till now and the Honourable Members have passed this Bill and until now is it not been implemented and we are the leaders to bring change to the people and I want to really congratulate Honourable Katana for this issue, for taking up this issue as his own. I know he is not suffering from any of this land but because he is a leader of the people he has taken it upon himself to come and help the people and I want to urge the Whole House to support him on this and as we walk with him on this journey. Thank you.*

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Members, I am afraid we are running out of time and I will give one minute each to Honourable Juma Seif Manuari first and lastly to Honourable Patrick Mbelle.

Hon. Juma Manuari: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa kila kitu katika hii dunia. Pili, Mheshimiwa Spika nimwambie ndugu yangu katana Allan Rogers kuwa utetezi katika watu wako ni muhimu zaidi kwa sababu wao ndio waliokupa nafasi ili uje uyazungumze yaliyoko kule chini. Mheshimiwa Spika mimi nataka kusema hivi tuna raha sana katika nchi yetu kwa saa hizi, tukona serekali ambayo tunajiita Broad-Based Government na nini serekali ambao imeundwa kumuangalia mnyonge wa chini. Tukiwa tutasimama na kusema kuwa milioni ya hamsi zilizotengwa zilipie Ardhi za Mombasa zote mimi nimwambie ndugu yangu Abdulswamad Shariff Nassir ni wakati arudi kwa ndugu Hassan Joho wakati alivyokuwa Gavana pale kwetu Likoni kulikuwa na *issue* kubwa ya Waitiki *land* lakini yule bwana mdogo alikwenda akakaa na Rais na akahakikisha mambo yote yale ambayo yalikuwa yanatusumbua pale Likoni yakatatuliwa kwa muda mchache.

Kwa hivyo hivi sasa hakuna haja ya kusema maneno mengi isipokuwa ni Gavana wetu achukue *initiative* yeye pamoja na viongozi ambao wako katika hii nchi waende mpaka kwa Mheshimiwa Rais kupitia waziri ndugu yetu Wahome na kupitia Gavana or aliyekuwa Gavana wa Mombasa ili shida ya Ardhi Mombasa itatulike kwa sababu sio tuu kwa ndugu yangu Rodgers peke yake hii ni *issue* ambayo iko Kenya nzima iko Mombasa nzima mimi mwenyewe ambaye nazungumza ni Mwakilishi wa Bofu lakini pia ni *squatter* cha ajabu cha nashangaa kuwa Mombasa tangu jadi hawa mababu zetu hizi Ardhi wali wauzia hawa Swahili maheka na maheka na maheka walikuwa wako wapi? Hawa Waswahili tangu zama hizo hatujafunguka akili twaambiwa Ardhi sijui ya nani Ardhi sijui ni ya nani kwani hili janga mimi naona Mheshimiwa Spika imefikia wakati sahihi kwa sababu wazee waliuzia wazee wenzao waliokua na pesa sisi vijana imefikia wakati wa kuyakomboa yale mashamba yarudi kwa mwananchi...

[Applause]

Ndugu yangu Rodgers yeye amepiga nduru kiasi chake cha nduru, lakini mimi nataka nikuambie ndugu yangu Rodgers pale mimi ambapo ni *squatter* niliwafuata wenye ardhi na wenye ardhi walirudi chini. Hivi sasa walitupa *beacon* nyumba kwa nyumba iliyobaki turudi chini tu *negotiate* na hawa watu na pia washatuambia kima wanachokitaka; mimi nimelibeba jukumu kuifuata ile Kamati Ardhi Fund na nimeongea na wao wakaniambia tutenge siku tuwaite pale *ground* waje wazungumze na wananchi tuende tumfuate *land owner* tuzungumze nae kile kima tuelewane. Sasa kwanzia hapo ikiwa tumeelewana na hii pesa kama iko na Gavana ama yule yote ambaye anahitajika kushughulika na ku *compensate* hii maneno ikiwa basi hatochukua jukumu kwanzia hapo na mimi pia ntapiga nduru kwa sababu nishamaliza, mimi nimetengeneza njia? Kamati inataka niite maana hatuna muda mrefu tukae nayo chini watupe mwelekeo, watufundishe, watuambie pesa ile tulioitenga katika Bunge hili tutaipata vipi na muambie Gavana wetu arudi Nairobi akakae na Rais warudi kama ni Kisauni. Kwa sababu kwa taarifa yako ndugu yangu Katana nimepata ripoti nyingine kuwa kwanzia Mtopanga mpaka Bamburi ni *plot* ya mtu moja. Kwanzia Mtopanga mpaka Bamburi ni shamba ya mtu moja; tulikuwa wapi sisi Wagiriama mpaka hii mashamba yakachukuliwa wakati huu tulikuwa wapi Mheshimiwa Spika? Mimi nimuambie tena nirudie kumwambia ndugu yangu Gavana kaa chini na Mheshimiwa Raisi na mawaziri na ndugu yetu '1GB' pia muweke ndani musuluhishe ile shida ya kule Kisauni na Mombasa kwa jumla. Kwa hayo mengi machache naona Mheshimiwa Spika wasegasega. Ahsante sana na Mungu atubariki.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Patrick Mbelle, you have one minute.

Hon. Mbelle: Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika kwanza nipongeze Mheshimiwa *1GB* Katana kwa kuleta hoja hii na kiukweli tangu tarehe 25 Oktobwa mwaka 2024 tulipitisha Ardhi Fund ndani ya Bunge hili na baadhi ya vipengee ya Ardhi Fund ni kinukuu kipengee cha tano ama Article 5 inasema kwamba, 'Asilimia tano ya mtaani tunasema maokoto lakini pesa zinazokusanywa kutoka na *land rights* zinafaa ziingie katika Ardhi Fund ili iweze kusaidia katika ununuzi na *administration* na mambo ya mashamba' kufikia leo hii Mheshimiwa Spika hakujawahi kutokea ama kuletwa Taarifa yoyote ama *report* ya kusema ni pesa ngapi tumekusanya kufikia leo ili iweze kufidia ama iweze kushughulikia maswala ya mashamba. Vile vile katika sheria hii ukienda katika ibara ya sita inasema kwamba serekali ya Kaunti itahusisha National Lands Commission (NLC) katika maswala ya ugavi ama kusuluhisha matatizo ya mashamba katika mji wetu Mombasa hasa hasa katika sehemu ya Kisauni.

Lakini kufikia leo Mheshimiwa Spika ningependa pia mimi kujua jee wizara yetu ya Ardhi imeshirikiana popote na NLC na kwa kiasi gani kuhakikisha kwamba leo hii tunapata majibu ya maswala ya mashamba. Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kulingana na sheria ndio mtu asiye akinukuu akisema tumeenda nje ya sheria kwa sababu yote haya ni maswala ya sheria. Ukienda katika Article 9 (4) inasema kwamba mashamba yatakayonunuliwa chini ya Ardhi Fund yatakuwa *charge* na kizungu inasema, '*...The titles acquired may be charged as security to guarantee the repayment to the person...*' ambaye atakuwa ametupea pesa Mheshimiwa Spika bado mpaka leo huwa nina dukuduku moyoni nikijiuliza hii Ardhi Fund kupitia kipengee hiki ambacho kilipita na Bunge hii ya kwamba iwapo Ardhi Fund itanunua shamba na shamba lile litatumika kama *security*, iwapo kama Kaunti tutakosa pesa ya kulipa mwenye ambaye anafaa tumlipe, jee watu wetu yale mashamba yatachukuliwa tena ama itakuwa ni mambo yale yale ya kwamba tumenunua tumewapea alafu yakaja yakachukuliwa?

Saa hii itakuwa si mambo yale tunasema Mwarabu tena itakuwa sasa ni nani atakuchua mashamba. Kwa hiyo Mheshimiwa Spika kuna muhimu wa Waziri wa Ardhi aletwe ndani ya Bunge hili ajibu haya maswala na iwapo utakuwa tumeona ameshindwa basi aende katika wizara ingine mwengine aletwe katika wizara ili tuweze kufanya maswala yatimilike. Mheshimiwa Spika inaniuma pia maswala Ardhi nikiongea kwa sababu katika Bunge hili nimeleta *Statements* na *Motion* mambo ya mashamba, mambo ya mashamba ya Bombo, mashamba ya Barawa, mashamba ya sehemu inaitwa Kashani, maswala ya Ugatuzi na majibu ninayopata mpaka leo hii ni majibu ambayo hayanipi chochote cha maana cha kusema kwamba tuko katika sehemu ya kuweza kuzuia matatizo haya. Lakini Mheshimiwa Spika alivyosema Waheshimiwa wenza ni kama tuna muda kwanzia sasa mpaka mwisho wa *term* hii ni muhimu kwamba tuanze kwanza ikiwezekana hata kesho waziri aje hapa aje atupee majibu baada ya hapo tujue kutoka hapo tunasuluhisha vipi haya maswala ya ardhi ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika nikimalizia inanisikitisha ya kwamba pia kuna ardhi ambazo zimepata hali miliki ndani ya Kisauni mfano kama vile Majaoni Mheshimiwa Spika cha kusikitisha ni kwamba baada ya kukaa katika mikutano mingi pamoja na wahusika katika Kaunti kuwaambia kwamba hati miliki zimetoka tuwapeeni hawa watu nafasi nyingi katika *Valuation roll* ili waweza kuchukua mikopo na mashamba yao, waweza kutumia mashamba yao kwa maswala tofauti lakini mpaka leo ni miaka imepita toka 2018 mpaka leo Mheshimiwa Spika hawajaingia katika *valuation roll* kumaanisha hawalipi ada kwa serikali ya Kaunti, serikali ya Kaunti inapoteza ada, pesa ile ingekusanywa ikanunulia wakashani shamba lakini hatui *collect*. Kwa hiyo Mheshimiwa Spika *I think there is a big problem with the Department of Lands* na ni muhimu kwamba sasa waje wakae chini na sisi tuwanoe msasa na baada ya hapo tupate majibu. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ni kupongeza ndugu yangu Allen Katana kwa kile ambacho umefanya leo hii na ni muhimu kwamba swala hili tulivulie njuga watu wetu waweze kupata nafuu ya kuweza kuishi katika sehemu zao.

Mheshimiwa Spika, mwisho nikimalizia kuna sehemu inaitwa Bombo. Bombo Mheshimiwa kuna shamba ambalo ni la serikali inaitwa GL na yako mengi katika sehemu ya Kisauni lakini kinachonishangaza ni kwamba Mheshimiwa Spika GL ni shamba ya serikali haihitaji Ardhi Fund kuweka pesa yeyote ni shamba ligawanywe watu wapewe waishi. Kwa hio inanishangaza ni kwa nini mpaka leo vitu kama shamba ya Ardhi Fund tuko miaka mitatu ndani na serikali ya Kaunti mbona tusifanye vitu kama hivyo tukamalizana na watu wakaishi katika mashamba yao watu waweze kuchukua mikopo wasomeshe watoto wao, wachukue mikopo wafanye biashara. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ni muhimu kuwa kuanzia leo hii ikiwezekana Bunge hili tusifanye biashara ingine tuanze maswala mambo ya mashamba tumalizane nayo mara moja kumaliza. Ahsante Mheshimiwa Spika.

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Point of information? Yes.

Hon. Noor: Thank you, Mr. Speaker for granting me. The information I have right now is that you can feel the Motion that is in the House. There is one of us who has expressed that he is a squatter within his land. Mr. Speaker, I would want you to take this opportunity to take us forward for what you are going to tell us; I urge you because this is a very important matter for us all with the people seated up there, I think the Speaker is going to make his decision. Tafadhali!

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): You are piling up a lot of pressure on me.

[Interruption]

Yes, are you up on a point of information? I want to wind up.

Hon. Mbele: Mr. Speaker, I just want to inform the House that we had passed the World Equitable Development Act just recently and part of the monies that we will get from the Act might be of use on us trying to acquire lands for our people. It is important to know that Mr. Speaker that until now we have places case example is Bamburi. We do not have even a public hospital and I am now forced to convince the people of Bamburi to use the monies that we will get from the World Equitable Development Act to buy land to build a hospital it is that disheartening Mr. Speaker that we now have to use monies for development to now buy or acquire land. So, it is just a point of information that our people need to know if all goes wrong the World Equitable Development Act gives them that reason and purpose to use their monies to now buy land for their own development. It was a point of information. Thank you, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Honourable Members, I want to believe that we have exhaustively discussed this Statement and I am pleased to note that this is for the first time I have never seen a Statement that has been discussed exhaustively in this House as this Statement. This shows the importance or rather the gravity of the matter at hand Honourable Members of the three roles that we have the legislative role of which we have all done with the adoption of the Ardhi Fund, the representation role that we are doing today whereby we are representing the people that elected us and lastly our oversight role that is we are holding the departments through our Committees accountable for the Acts and the laws that we have passed. Honourable Members, allow me to note the following concerning this matter, and I now direct that the Committee on Lands Housing Urban and Planning.... is the Chairperson present?

[Silence]

The Chairperson is not present. However, I can see that the Members are present. Please, the Members and the Chairperson please note that...

[Low Consultations]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Florence, are you the Vice-chair of this Committee?

Hon. Mkanjala: ...*[Inaudible]*.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Pardon?

Hon. Mkanjala: *[inaudible]*.

[Hon. Member off microphone]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): I was not aware of that, congratulations for your position. Honourable Members, the Committee on Lands, Housing and

Urban Planning is directed to investigate the matter that we have just discussed through the statement together with the Ardhi Fund Board and report back to this Honourable House without fail in two weeks time. Also, in that meeting we will also give an opportunity to invite the stakeholders to be part and parcel of that Committee meeting and the findings of that meeting should be made available to this House in two weeks time. So, Honourable Members without further ado Honourable Katana are you satisfied with that? I will give you a parting shot.

Hon. Katana: I am most obliged Mr. Speaker and I also want to thank the Honourable Members for their contribution and it's my sincere hope that we shall win this battle. I thank you Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir): Thank you. For the avoidance of doubt, I have said that the Committee calls upon the CECM in charge the department, the Ardhi Fund Board as well as the stakeholders in a meeting that these issues are discussed and the report comes back to this House. Yes, Clerk?

ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until Tuesday 19th August, 2025 at 2:30p.m. Thank you.

The House rose at 12:45p.m.